TANGAZO LA SERIKALI Na. 50X la tarehe. 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA. 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE HUDUMA YA KIHANDISI NA HUDUMA ZA UJENZI KATIKA KATIKA UJENZI WA MRADI WA UANZISHAJI WA KIWANDA CHA KUZALISHA GYPSUM PLASTER NA GYPSUM PLASTER BOARD NA UPANUZI WAKE KWA KAMPUNI YA KNAUF GYPSUM TANZANIA LIMITED YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Huduma ya kihandisi na Huduma za ujenzi katika Ujenzi wa Mradi wa Uanzishaji wa Kiwanda cha Kuzalisha Gypsum Plaster na Gypsum Plaster Board na Upanuzi wake kwa Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania Limited ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 27 Juni, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio kwenye huduma ya kihandisi na huduma ya Ujenzi katika ujenzi wa mradi wa uanzishaji wa kiwanda cha kuzalisha gypsum plaster na gypsum plaster board na upanuzi wake inasemehewa

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo tarehe 31 Disemba, 2026 kwa mujibu wa kifungu cha 3.3 cha mkataba wa utekelezaji baina ya kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania Limited na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania wa tarehe 29 Machi, 2022.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*